BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Saba – Tarehe 05 Disemba, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) kwa mwaka 2023/2024.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016 na Kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kuweka Masharti Bora ya Kusimamia na Kudhibiti Ununuzi wa Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Udhibiti wa Mfumo wa Utoaji Leseni za Biashara, Nam. 13 ya 2013 na Kutunga Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Utoaji Leseni za Biashara Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) kwa mwaka 2023/2024.

## III. HOJA YA MJUMBE:

**Mhe. Juma Ali Khatib**

Hoja Binafsi ya Mjumbe kuhusu Kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi) kwa Mafanikio ya miaka minne ya uongozi wake.

## IV. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

91. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Tuna haja ya kuipongeza Serikali pale inapofanya uamuzi wa kusitisha na kuzuia leseni kwa zile baa ambazo hazina vizuizi sauti (*sound proof*).

    (a) Je, hadi hivi sasa Zanzibar kuna baa ngapi ambazo zimesajiliwa rasmi.

    (b) Je, ni vigezo gani na utaratibu upi hutumika kuzisajili baa hizo.

    (c) Je, ni baa ngapi kati ya hizo zimetimiza sharti la vizuizi sauti na ngapi bado hazijatimiza.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

128. MHESHIMIWA CHUM KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

     Kwa kuwa Serikali inahamasisha juu ya matumizi ya risiti za kielektroniki kwa mnunuzi na muuzaji.

     Je, Serikali ina utaratibu gani kwa matumizi ya mashine hizi na kuachana na risiti za mikono.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

49. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Kwa kuwa tumeanza mfumo mpya wa kuwapima wanafunzi kwa umahiri.

    Ni lini Serikali itaandaa zawadi maalumu kwa wanafunzi bora watakaobuni vitu mbali mbali vyenye faida kwa jamii.

50. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    (a) Kwa mujibu wa mtaala mpya wa kupima umahiri, je walimu wa masomo ya TEHAMA, Hesabati, na Kiengereza wanatakiwa wasomeshe vipindi vingapi kwa mwezi kwa ngazi ya shule za msingi.

    (b) Ni kwa kiasi gani utaratibu huo unafuatwa ipasavyo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

69. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Ni yepi mafanikio na matarajio zaidi ya Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika kuifungua Pemba hususani kwenye Sekta ya Mawasiliano, Usafiri na Utalii.

70. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    (a) Tathmini iko vipi mpaka sasa juu ya mafanikio ya uwekezaji katika sekta ya Bandari na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

    (b) Nini matarajio ya uwekezaji huo kwa siku za baadae.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

40. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Profesa Said Ahmed Mohamed licha ya kuwa nguli wa utunzi wa vitabu vya tamthilia, riwaya na ushairi alikuwa pia ni mtunzi, mtia sauti na muimbaji katika kikundi cha Nad Ikhwan Safaa.

(a) Kwa namna gani Serikali imeiandika katika kumbukumbu na kuenzi historia yake.

(b) Yupo wapi kwa sasa nguli wa fasihi duniani Shafi Adam Shafi.

(c) Yupo wapi bingwa wa fasihi duniani kwa ujumla Profesa Mohamed Suleiman.

41. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

ZIFF ni tamasha la filamu lililoijengea sifa na heshima kubwa nchi yetu duniani kupitia tasnia ya filamu.

(a) Kwa nini mpaka leo Zanzibar tukiwa kama wenyeji kwa miaka mingi bado tupo nyuma sana katika ulimwengu huu wa filamu.

(b) Sababu zipi zinazopelekea filamu za Bongo 'Movies' kufanya vizuri kuliko filamu za Zenji 'Movies'.

(c) Nini matarajio ya kuiweka Zanzibar kwenye muelekeo mzuri wa ulimwengu wa filamu.

**Wizara ya Afya:**

94. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kiasi gani agizo la Mhe. Makamu wa Pili wa Rais la kuutaka uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha malipo ya posho za madaktari na manesi wanaoingia usiku limetekelezwa ipasavyo.

118. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ongezeko la maduka ya dawa yamerahisisha upatikanaji wa dawa za binadamu, lakini pia yameongeza hatari ya madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi hayo. Hali hii imepelekea tatizo kubwa la utumiaji wa dawa kiholela.

(a) Kwa tathimini iliyofanywa na Wizara yako, hali ya utumiaji wa dawa kiholela iko vipi hapa Zanzibar.

(b) Ni miongozo gani ya kitaalamu ambayo Serikali imetoa kwa wamiliki wa maduka ya dawa ili kupunguza athari za utumiaji wa dawa kiholela.

(c) Ni athari zipi zinazoweza kutokea kutokana na utumiaji wa dawa za binadamu kiholela.

<u>**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**</u>

26. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Ni kwa kiasi gani azma ya kuifanya Zanzibar kuwa kituo kikuu cha kusambaza mafuta na gesi (hub) katika ukanda mzima wa Afrika Mashariki inatekelezwa.

<u>**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**</u>

54. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Tathmini iko vipi juu ya matukio ya hivi karibuni ya wimbi la kupotea watoto.

126. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Kumekuwa na ongezeko kubwa na vituo vya malezi ya kutwa (Day Care Centres) kwa watoto wadogo hapa Zanzibar. Vituo hivi vimekuwa msaada mkubwa kwa watu tofauti ambao huvitumia kuwaacha watoto ili kuweza kufanya shughuli zao za kila siku za kujiongezea kipato.

(a) Kwa kuzingatia tathmini iliyofanywa na Wizara yako, ni vituo vingapi ambavyo vimepata usajili na kutambulika hapa Zanzibar.

(b) Je, ni upi muongozo wa kuanzisha vituo vya malezi ya kutwa hapa Zanzibar.

(c) Ni jitihada gani Serikali inatumia kuhakikisha vituo hivi vinafuata maadili na desturi za nchi yetu.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

17. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Marekebisho ya Sheria ya Kulinda Haki za Wanyama yamekwama wapi mpaka sasa.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

87. MHESHIMWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Tathmini iko vipi kuhusu ujio wa ziara maalumu ya Mufti Menk kwa muktadha mzima wa kuukuza Utalii wa Kiislamu (Halal Tourism) hapa Zanzibar.

116. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Bwawa la Bwawani ni moja ya eneo muhimu kwa mazalio ya ndege wa aina mbali mbali wanaotoka sehemu tofauti duniani na kupelekea kuwa kivutio kizuri kwa watalii wanaoshughulika na utalii wa ndege. Licha ya eneo hilo kuwa na historia kubwa lipo katika hali mbaya ya kimazingira.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kulitunza eneo hilo ili kuepusha athari mbaya za kimazingira.

(b) Je, ni aina ngapi za ndege zinapatikana katika Bwawa hilo.

(c) Je, Serikali inatumia mkakati gani kulitangaza eneo hilo ili kuongeza utalii wa ndege.

## V. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) kwa mwaka 2023/2024.

## VI. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016 na Kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kuweka Masharti Bora ya Kusimamia na Kudhibiti Ununuzi wa Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Udhibiti wa Mfumo wa Utoaji Leseni za Biashara, Nam. 13 ya 2013 na Kutunga Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Utoaji Leseni za Biashara Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

## VII. HOJA YA MJUMBE:

**Mhe. Juma Ali Khatib**

Hoja Binafsi ya Mjumbe kuhusu Kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi) kwa Mafanikio ya miaka minne ya uongozi wake.

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**

**Zanzibar,**
**05 Disemba, 2024.**